JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Anwani ya simu "AFYA", **DODOMA**
Simu nambari: **255 26 232367**
Fax:2137591

(Barua zote ziandikwe kwa
Katibu Mkuu)

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Kitivo cha Sanaa na Sayansi
ya Maendeleo ya Jamii,
S.L.P. 743,
Jengo na 11
40478 DODOMA.

Kumb. Na. JB 33/333/01/AMO/BUG/17/JI…. **25 Septemba, 2017**

Kwa…….

……...

KK…….

……

Yah: MAFUNZO KATIKA VYUO VYA AFYA KWA MWAKA WA MASOMO 2017/18

Napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza na kukutaarifu kwamba Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) imekuchagua kujiunga na mafunzo katika kozi ya Utabibu (Clinical Medicine) ngazi ya **Stashahada ya Juu katika** Chuo cha **Bugando.** Mafunzo haya ni ya miaka miwili (**2)**.

Masomo yataanza tarehe **29/10/2017.** Kwa barua hii, unatakiwa kuripoti chuoni tarehe **22/10/2017.** Kutokana na uchache wa nafasi za masomo, nafasi yako itahesabika kupotea kabisa na kujazwa na mtu mwingine endapo hautafika katika kipindi cha wiki mbili baada ya masomo kuanza. Hivyo, endapo utakuwa bado na nia ya kujiunga na mafunzo ya fani hii, itakubidi kuomba nafasi upya mwaka wa masomo **2018/2019.**

Mwanafunzi atakayekuwa tayari kwenda Chuoni baada ya kuahirisha masomo anatakiwa kutoa taarifa kwa Mkuu wa Chuo kabla ya mwezi Februari ya mwaka 2018. Taarifa hizo zinatakiwa zipokelewe Wizarani ifikapo mwezi Machi, 2018.

Gharama za chuo zinafuata utaratibu wa uchangiaji ambao hutolewa kila mwaka. Mchanganuo wa gharama hizo umeainishwa kwenye jedwali hapa chini:

Na	**Kipengele**	**GHARAMA KWA FEDHA ZA KITANZANIA**	
		Wanafunzi wa Bweni	**Wanafunzi wa Kutwa**
1.	Mafunzo	450,000.00	450,000.00
2.	Mitihani ya Ndani	150,000.00	150,000.00
3.	Usajili	20,000.00	20,000.00
4.	Michezo	10,000.00	10,000.00
5.	Fedha ya Dharura	10,000.00	10,000.00
6.	Cheti cha Kuhitimu	20,000,00	20,000,00
7.	**Malazi	150,000.00	0.00
8.	Gharama za Matibabu	50,400.00	50,400.00
9.	Mitihani ya Kitaifa	150,000.00	150,000.00
10.	NACTE Quality Assurance	15,000.00	15,000.00
11.	Mafunzo kwa Vitendo (Community Field Study)	300,000.00	300,000.00
12.	Practicum Guide and Procedure Book	80,000.00	80,000.00

13.	Chakula (Utajitegemea)	0.00	0.00
JUMLA KUU (Wasiokuwa na Bima ya Afya)		**1,405,400.00**	**1,255,400.00**
JUMLA KUU (Walio na Bima ya Afya)		**1,355,000.00**	**1,205,000.00**

**** Kiwango kinachotakiwa kulipwa kwa ajili ya Malazi kitazingatia kiwango kitakachokuwa kimepangwa na Bugando Medical Centre (BMC).**

Fedha ya mitihani ya kitaifa inatakiwa kulipwa kwenye Akaunti yenye Nambari: 20110007946, yenye jina 'Application and Examination Fee Account', iliyoko NMB Bank House. Inasisitizwa kwamba ni fedha ya mitihani peke yake ndiyo italipwa kwenye akaunti hiyo, Fedha nyingine zote zinalipwa chuoni.

Mwanafunzi atajitegemea chakula, gharama ya chakula kwa mwanafunzi kwa siku inakadiriwa kuwa kiasi kisichopungua shilingi 4,000/= (Shilingi Elfu Nne tu). Hivyo mzazi/mlezi au mfadhili atatakiwa kulipa gharama hizi moja kwa moja kwa mwanafunzi mwenyewe kulingana na muda atakaokuwepo chuoni.

Ieleweke kwamba gharama za matibabu zitatolewa na wale ambao hawana Bima ya Afya, ili kuwawezesha kujiunga na Mfuko huo wakati wote watakapokuwa chuoni. Hivyo jumla ya fedha ya uchangiaji kwa wasiokuwa na Bima ya Afya itakuwa ni **Shilingi 1, 405,400/= (Milioni Moja, Mia Nne na Tano Elfu na Mia Nne tu kitalipwa na mwanafunzi wa bweni)**.Aidha kiasi cha **shillingi 1,255,400/= (Milioni Moja, Mia Mbili na Hamsini na Tano Elfu na Mia Nne tu kitalipwa na mwanafunzi wa kutwa).** Fedha ya matibabu itakusanywa na Mkuu wa chuo na kuwasilishwa kwa Mratibu wa Bima ya Afya wa Kanda, ambaye atafanya utaratibu wa kutoa kadi za Bima ya afya kwa wanafunzi waliochangia. Fedha hii itatolewa na mwanafunzi kila mwaka na ni lazima ilipwe na mwanafunzi anaporipoti chuoni kwa mara ya kwanza.

Wanafunzi walio na Bima za afya watatumia kadi zao za Bima kwa matibabu wanapokuwa chuoni. Hivyo gharama yao ya uchangiaji ni **1, 355,000/= (Milioni Moja, Mia Tatu na Hamsini na Tano Elfu tu kitalipwa na mwanafunzi wa bweni) na Shillingi 1,205, 000/= (Millioni Moja, Mia Mbili na Tano Elfu tu kwa mwanafunzi wa kutwa).**

Mwanafunzi wanaofanya mafunzo kwa vitendo ndani ya hospitali watatakiwa kuchangia **shilingi 80,000/= (Elfu Themanini tu) (**ikiwa ni gharama za uchangiaji kwa uchapishaji wa 'Practical Procedure books' na 'Practicum Guide'). Malipo haya yanafanyika mara moja tu katika kipindi chote cha masomo.

Mwanafunzi anatakiwa kuchangia gharama za mafunzo kwa vitendo kwa kulipia kiasi cha shilingi **300,000/- (Mia Tatu Elfu tu)** kila mwaka. Fedha hizi utapewa muda utakapofika wa kwenda kwa ajili ya mazoezi kwa vitendo (field attachment)

Kabla ya kwenda chuoni hakikisha umepimwa afya yako na Daktari ambaye atajaza fomu iliyoambatanishwa na barua hii. Fomu hiyo utaikabidhi kwa Mkuu wa Chuo mara tu ufikapo chuoni. Wakati wote utakapokuwa chuoni unatakiwa kutii sheria na taratibu za nchi na zile zilizowekwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Vilevile ieleweke kwamba masuala yote ya mwanafunzi anapokuwa chuoni yatashughulikiwa na Uongozi wa chuo, endapo itakuwa lazima suala la mwanafunzi kushughulikiwa na Makao Makuu ya Wizara kupitia Idara ya Mafunzo, basi maombi au matatizo yote yapitie kwa Mkuu wa Chuo kabla ya kuwasilishwa Wizarani.

Usafiri wa kwenda na kurudi chuoni ni gharama ya mwanafunzi na wala si jukumu la Wizara. Hakikisha unakuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi yako madogo madogo kwa kipindi chote utakapokuwa chuoni.

Nafasi uliyopewa ni mali ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na haibadilishwi kwa mtu yeyote. Endapo hutaweza kwenda masomoni toa taarifa Wizarani ukiambatanisha na nakala halisi (Original) ya barua hii ndani ya wiki mbili. Kwa kufanya hivyo, utaiwezesha Wizara kutoa nafasi hii ya masomo kwa mtu mwingine.
Kila mwanafunzi anatakiwa kwenda chuoni na vifaa vifuatavyo:-

Kabla ya kwenda chuoni hakikisha afya yako imepimwa na kupata cheti kutoka kwa Daktari. Cheti hicho itakubidi ukikabidhi kwa Mkuu wa Chuo mara tu ufikapo

Kila mwanafunzi anatakiwa kwenda chuoni na vyeti/Cheti halisi cha kumaliza elimu ya sekondari kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa na cheti cha kuhitimu mafunzoya Taaluma. Hakuna mwanafunzi atakayepokelewa chuoni bila kuwa na cheti halisi. Endapo utakamatwa na cheti cha kughushi, utashitakiwa kisheria na chuo hakitawajibika kukurudishia gharama yoyote ikiwa ni pamoja na gharama ya uchangiaji.

SARE:

- **Mwanamke:**
  - Mavazi ambayo yaliruhusiwa kwa mujibu wa waraka wa utumishi wa mwaka 2012, viatu vyeupe, vyeusi au kahawia vyenye visigino vifupi. Makoti mawili (2) meupe na masafi. Koti moja liwe na mikono mirefu na lingine mikono mifupi. 'Jeans' siyo vazi la kuvaa darasani au wakati wa mazoezi kwa vitendo hospitalini.
- **Mwanaume**:
  Mavazi ambayo yaliruhusiwa kwa mujibu wa waraka wa utumishi wa mwaka 2012, viatu vyeupe, vyeusi au kahawia vyenye visigino vifupi. Makoti mawili (2) meupe na masafi. Koti moja liwe na mikono mirefu na lingine mikono mifupi. 'Jeans' siyo vazi la kuvaa darasani au wakati wa mazoezi kwa vitendo hospitalini.

VIFAA/VITU VINGINE VINAVYOHITAJIKA

1. Kifaa cha kupimia mapigo ya moyo (Stethoscope)
2. Kifaa cha kupimia msukumo wa Damu (BP Machine)
3. Kifaa cha kupimia joto la mwili (Thermomerter)
4. 'Patella Hammer'
5. Tochi ndogo
6. Nguo za michezo mbali mbali
7. Ndoo ya maji aina ya "Plastic"
8. 'Ream' moja ya Karatasi
9. Picha nne(4) Passport size kwa ajili ya kumbukumbu
10. Vitabu vya rejea vya kozi husika inapowezekana
11. Vifaa vya kuandikia kwa mfano madaftari, kalamu, rula n.k
12. Mwamvuli au koti la mvua kwa wale watakaokuwa kwenye kanda ya mvua nyingi
13. Shuka 4, mto 1, blanketi 1, chandarua na taulo.

SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE

1. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa katika mazingira ya shule ifikapo saa 1.00 jioni siku za kawaida na saa 3.00 usiku siku za mwisho wa wiki na sikukuu (Jumamosi na Jumapili). Wanafunzi atakayekuwa nje ya chuo zaidi ya muda uliotajwa hapo juu kwa sababu maalum anatakiwa kupata ruhusa maalum kwa maandishi (gate pass) toka kwa Mkuu wa chuo au Mlezi wa chuo.
2. Kila mwanafunzi atawajibika kwa usafi wa chumba anachoishi na usafi wa mazingira ya chuo. Hairuhusiwi kubandika magazeti/vipande vya magazeti au picha kwenye kuta za majengo ya chuo.
3. Kila mwanafunzi atatakiwa kushiriki kikamilifu katika michezo na shughuli nyingine za chuo kama zitakavyoelekezwa na uongozi wa chuo.
4. Wageni hawaruhusiwi kuingia kwenye vyumba vya wanafunzi. Endapo mgeni/wageni watahitaji kuzunguka na kuangalia maeneo ya chuo, watatakiwa kupata kibali toka kwa Mkuu wa chuo.
5. Wageni hawaruhusiwi kuonana na wanafunzi wakati wa vipindi na wanatakiwa kuwa wameondoka kwenye maeneo ya chuo ifikapo saa 12 jioni
6. Wageni wanatakiwa kuandikisha katika kitabu cha wageni, kinachoonesha jina la mgeni, mahali anakotoka, uhusiano na mwanafunzi anayemtembelea, anuani yake na muda wa kuingia na kutoka.
7. Hairuhusiwi wanafunzi wa kiume kwenda kwenye vyumba vya wanafunzi wa kike na vivyo hivyo kwa wanafunzi wa kike kwenda kwenye vyumba vya wanafunzi wa kiume.
8. Wanafunzi wanatakiwa kuvaa sare za chuo wakati wote wanapokuwa darasani, katika mafunzo kwa vitendo hospitalini na shughuli nyingine za chuo kama itakavyoelekezwa na uongozi wa chuo.
9. Wanafunzi wanatakiwa kuvaa koti jeupe na safi wakati wote anapokuwa katika mafunzo kwa vitendo au zamu hospitalini.
10. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa nguo za heshima wakati wote anapokuwa chuoni au anapokuwa kwenye mafunzo kwa vitendo hospitalini. Zingatia waraka wa mavazi uliotolewa na Idara kuu ya Utumishi mwaka 2011.
11. Wanafunzi wa kiume hawaruhusiwi kufuga ndevu, mustachi, kucha, kusuka nywele na kupaka rangi kwenye kucha na nywele au kuvaa mavazi yasiyoendana na jinsi yake.

12. Wanafunzi wa kike wasuke nywele vizuri ambazo hazitaingilia huduma za kitabibu zinazotolewa wakati wa mafunzo kama rasta ndefu au mtindo wowote wa nywele zakuning'inia. Aidha, ufugaji wa kucha, rangi za kucha zinazobanduka, rangi za mdomo na rangi za kope sio sehemu ya sare za shule, haziruhusiwi wakati wa muda wa darasani na mafunzo kwa vitendo hospitalini.
13. Pombe hairuhusiwi katika mazingira ya chuo. Aidha, matumizi ya pombe na sigara hayaruhusiwi, na madawa ya kulevya na bangi kuvunja sheria na utashitakiwa na jamhuri.
14. Upigaji wa kelele bila sababu ya msingi haurusiwi katika maeneo ya chuo au hospitali.
15. Wanafunzi wote wanawajibika kutunza vifaa na majengo ya chuo. Ni marufuku kujihusisha na uharibifu wa aina yeyote. Aidha, mwanafunzi atakayeharibu mali ya chuo, atawajibika kuilipa pamoja na kuchukuliwa hatua za kinidhamu.
16. Hairuhusiwi kukaa na silaha ya aina yeyote, ikiwemo kisu au panga.
17. Mwanafunzi yeyote mwenye vifaa vya umeme mdogo kama Televisheni ndogo, kompyuta, radio na pasi, atoe taarifa kwa Mkuu/Mlezi wa chuo. Aidha, mwanafunzi haruhusiwi kuwa na jiko la umeme au lile la mafuta ya taa chumbani.
18. Mwanafunzi anayeumwa anatakiwa kutoa taarifa kwa Mkuu/Mlezi wa chuo. Kila mwanafunzi anayehudhuria matibabu awe na 'sick-sheet' kabla ya kupata matibabu. Isipokuwa pale tu matibabu yake yanakuwa ya dharura na upatikanaji wa 'sick-sheet' ni mgumu. Hata hivyo, bado mwanafunzi huyo atatakiwa kujaziwa 'sick-sheet' baada ya matibabu. 'Sick-sheet' zote zinatakiwa kurudishwa kwa Mkuu/Mlezi wa chuo na kutunzwa kwenye majalada ya kumbukumbu za wanafunzi husika.
19. Mwanafunzi haruhusiwi kushiriki katika kutenda makosa ya jinai. Aidha, mwanafunzi yeyote atakayethibitika kushiriki kutenda kosa ya jinai atasitishwa masomo na kuamuriwa kuondoka eneo la chuo haraka iwezekanavyo.
20. Mwanafunzi anatakiwa kushiriki kikamilifu katika matukio yote yanayohusu mafunzo bila kukosa. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuondoka eneo la chuo/mafunzo bila taarifa ya maandishi kutoka kwa mkuu wa chuo/mlezi wa wanafunzi.
21. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha ya matusi au udhalilishaji, kupigana, kufanya migomo na maandamano bila kufuata utaratibu, kuiba na kumiliki mali kinyume cha sheria.
22. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya vitendo vyenye kushawishi ngono ndani ya majengo ya chuo na hospitali
23. Mwanafunzi anaruhusiwa kushiriki hafla za kiimani zinazohusiana na imani ya dini mbalimbali baada ya kuwa amepata kibali kutoka kwa mkuu wa chuo.
24. Mwanafunzi haruhusiwi kushiriki au kuendesha harakati za kisiasa chuoni
25. Mwanafunzi wa kike atakayedhihirika kuwa na mimba toka kwa mwanafunzi mwenziye au amempa mwanafunzi mwenzie mimba basi watarudishwa nyumbani kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.
26. Mwanafunzi anatakiwa kufuata taratibu zote wakati wa mitihani. Aidha kushiriki katika kugushi matokeo ya mitihani, nyaraka za serikali hakutavumiliwa, na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wahusika.

ANGALIZO: Uvunjaji wa taratibu zilizoainishwa hapa juu unaendana na adhabu, ambazo zimeelekezwa katika kitabu cha maadili ya wanafunzi walioko katika vyuo vya afya kilichotolewa, na wizara ya afya mwaka 2004 (Disciplinary Code for Students in Health Training Institutions Revised 2004).

Ninakutakia kila la kheri katika masomo yako.

Dkt. Otilia F. Gowelle
K.n.y: KATIBU MKUU (AFYA)

M.F.M. 14

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PART A

FROM: DHR
MINISTRY OF HEALTH, COMMUNITY DEVELOPMENT, GENDER, ELDERLY AND CHILDREN
P.O. BOX 743,
40478 DODOMA

TO: MEDICAL OFFICER,

……

……

Station……

Mr. / Mrs /Miss……
Please examine the above named as to *his/her fitness for appointment/re-engagement as a student.

Date 25 September, 2017 (Signed Dr O.F Gowelle)

PART B

MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by a Medical Officer)

I have examined the above and consider that *he/she is physically fit for appointment:
Re-engagement as above.

Date…….....2017 Signature…….

Station……

Designation…….

***Delete as necessary**